**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**
**(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

**MKOA WA KILIMANJARO**
Simu : 27-29 74369
Fax : 27- 29 74368
Email: ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
**HAI KILIMANJARO**

Kumb.Na.LG/S.10/7/50

Tarehe: 28/03/2025

## TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Hai anawatangazia Wakazi wa Wilaya ya Hai wenye sifa na nia ya kufanya kazi za kujitolea kwa mkataba kwa kada ya udereva katika kituo cha Afya Kisiki na Longoi kuomba nafasi mbili (02) kama ilivyo ainishwa hapa chini.

### 1 Dereva (nafasi 2)

**Sifa za mwombaji:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne (IV)
- Leseni ya Daraja E au C, ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

**Majukumu ya kazi ya Udereva**

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
ii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
iii. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
iv. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
v. Kufanya usafi wa gari na
vi. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

**MSHAHARA**
Waombaji watakaopata nafasi na kupewa mkataba wa kazi watalipwa mshahara asilimia hamsini (50%) ya mshahara wa Serikali kulingana na kada husika.

**SIFA/MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI**

1. Awe Raia wa Tanzania na Mkazi wa Wilaya ya Hai
2. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 45
3. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali
4. Kila mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho wa taifa (NIDA)
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae)yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika
6. Testmonial" "Provisional Results" Statement of result hati ya matokeo ya kidato cha Nne na kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**)
8. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **10 Aprili, 2025**
9. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
**HAI – KILIMANJARO**

10. Maombi yatumwe kwa njia ya posta au yawasilishwe moja kwa moja kwenye Masjala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-**

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**HAI**